# *Utaratibu Wa Kanisa*

Tumemaliza hivi punde ule mkutano mkubwa wa siku tano usiku kwenye Maskani, ambapo, kwa neema ya Mungu na kwa msaada Wake, nimejaribu sana, kwa Maandiko, kuliweka Kanisa la Bwana Yesu Kristo katika Utaratibu, kama tunavyoamini katika Maskani ya Branham.

2 Jambo la kwanza ninalotaka kusema ni kwamba mchungaji ndiye mwenye mamlaka kamili katika Maskani haya, nisipokuwepo, nami namtumainia tu yeye ninaporudi. Kwa hivyo yeye ndiye aliye na mamlaka ya kugeuza ama kufanya cho chote anachodhania kinafaa kabisa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, nisipokuwepo.

3 Sisi tunaamini katika Kanisa la kimitume, tukifundisha Baraka za kimitume kwa ajili ya watu wa siku hizi. Tunaamini katika Injili yote, na kuamini ya kwamba ishara zote na maajabu zilizonenwa, na Bwana wetu Yesu Kristo, zitaandamana na Kanisa Lake hata atakaporudi. Tunaamini katika mambo hayo, na kuamini ya kwamba yanapaswa kuwekwa katika utaratibu, ya kwamba Kanisa lina utaratibu Wake. Kila kanisa lina mafundisho yake, taratibu na nidhamu.

4 Kanisa letu halina washiriki wa kujiunga. Tunaamini ya kwamba Kanisa lote la Mungu aliye hai, wao ni ndugu na dada zetu; na kwamba watu wote wamekaribishwa daima, bila kujali wao ni wa dhehebu gani, katika Maskani ya Branham, kwenye Barabara ya 8 na ya Penn Jeffersonville, Indiana.

5 Tunaamini katika "kuhesabiwa haki kwa imani," Warumi 5:1. Tunaamini ya kwamba, baada ya mtu kuhesabiwa haki kwa imani, yeye ana amani kwa Bwana Yesu Kristo. Bali inawezekana kwamba mtu yuyo huyo anaweza kuwa na tabia kama vile kunywa pombe, kuvata sigara, na kutenda mambo ambayo hayampasi kutenda, tabia baya za kimwili.

6 Kisha tunaamini Damu ya Bwana Yesu Kristo inamtakasa mtu huyu kwa utumishi wa Bwana. Na, hiyo ni kusema, tunaamini katika "utakaso" kulingana na Waebrania 13:12 na 13, "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa Damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango." Nasi tunaamini ya kwamba utakaso umefundishwa katika Agano Jipya, na unakusudiwa kwa waamini wote wa wakati wote wa Agano Jipya, ambamo tunaishi sasa. Pia tunaamini ya kwamba baada ya huyo mtu kutakaswa, tabia mbaya humwacha mtu huyo.

7 Yeye anamwanimi Bwana Yesu Kristo, na tabia zake zimeondoka, tunaamini ya kwamba basi yeye yuko tayari kwa "ubatizo wa Roho Mtakatifu," ambaye hufa kama kujazwa kwa mwamini. Kisha wakati huyo mwamini . . .

8 Hiyo ni kama tu, kama vile nimeifundisha mara nyingi, kama kuitwaa gilasi kutoka kwenye kitalu cha kuku. Kuihesabia haki, ni kuitwaa, tayari kwa matumizi, unakusudia hilo moyoni. Hivyo ndivyo Mungu anavyomtendea mwenye dhambi. Yeye yu angali mchafu.

9 Kisha anasafishwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Basi neno *takasa* lina maana mbili, maana yake ni, "kusafishwa, na kutengwa kwa ajili ya utumishi." Katika Agano la Kale, madhabahu yalikitakasa chombo, kisha kikatengwa kwa ajili ya utumishi.

10 Tunaamini ya kwamba Roho Mtakatifu anakitumikisha chombo hicho hicho. Ya kwamba, Roho Mtakatifu si hatua nyingine ya neema, bali ni ongezeko la neema ile ile, ambayo humjaa mwamini kufikia kiwango ambacho ishara na maajabu, kama vile zile karama za kimitume ambazo zimetajwa katika Wakorintho wa Kwanza 12, zinajidhihirisha zenyewe kupitia kwa mwamini huyu, Roho Mtakatifu anapoingia kuchukua hizo karama.

11 Naamini ya kwamba Maandiko yanafundisha ya kwamba "karama, wala mwito, hizina majuto," ya kwamba tunapozaliwa katika ulimwengu huu, tunatumwa hapa kwa kusudi moja, hiyo ni kusema, la Mungu. Na ya kwamba, hata kabla hatujakuwa watu wazima, tukali watoto, zile karama tulizo nazo za Mungu zimo ndani yetu wakati huo, na ni kujazwa tu na Roho Mtakatifu kunakozifanya hizi karama kuanza kutenda kazi; bali sisi huwa nazo tangu mwanzo, kama vile walimu, na mitume, na—na manabii, na zile karama za lugha, na zile karama tisa za kiroho kulingana na Wakorintho wa Kwanza 12. Sasa, tunaamini ya kwamba karama hizi zinatenda kazi siku hizi, nazo zinapaswa kuwa katika kila kanisa la mahali hapo.

12 Ijapokuwa, katika hayo, tumeona, kote ulimwenguni, ya kwamba kuna ushupavu mwingi wa dini unaoandamana na watu wanaokiri kuwa ni waamini wa kimitume. Kama ilivyo katika huduma zingine takatifu, na kadhalika, sisi tuna washupavu wa dini. Hiyo imekuwa hivyo kila wakati, tumekuwa na hao katika nyakati zote. Walikuwa nao katika siku za mitume; na kama Paulo alivyosema pale, jinsi ambavyo wengine walikuwa wamekuja na "kuwashawishi, kufuata mafundisho mengine," na kadhalika. Bali katika Mafundisho yake, yeye alisema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni angefundisha jambo lingine lo lote," isipokuwa yale yeye alikuwa amefundisha, "na alaaniwe."

13 Kwa hivyo, sisi, kama Maskani ya Branham, kwenye Barabara ya 8 na ya Penn hapa, hujaribu kufuata Mafundisho ya Agano Jipya. Kwa kuwa, tunaamini Hayo, "Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu." Naye mtume Paulo alikuwa chombo kilichoitwa na kuteuliwa, kwa kuchaguliwa na

Mungu, kutumwa katika Kanisa la Kimataifa, kuliweka katika utaratibu.

14 Sasa, tunaamini katika “ubatizo wa maji,” katika Maskani ya Branham, kwa kutiwa majini kabisa “katika Jina Lake Bwana Yesu Kristo,” ambalo ni Fundisho la kimitume la Biblia. Na washiriki wetu wote, ama watu wanaohudhuria Maskani ya Branham, wanaotaka hayo, wanaweza wakati wo wote (kuomba kufanyiwa hivyo) kutiwa majini kabisa katika Jina Lake Bwana Yesu. Hebu na amwone mchungaji, iwapo wao wamekwisha kutubu, na kumwamini Bwana Yesu Kristo, kisha mchungaji, upesi iwezekanavyo, hata wakati uo huo akiweza, awabatize mara moja. Hili huwaingiza katika ushirika wa waamini. Tunaamini ya kwamba kwa ubatizo wa maji tunaingizwa katika ushirika.

15 Bali, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunafanywa washiriki, tukiwa washiriki wa Mwili wa Yesu Kristo, ambao uko ulimwenguni kote.

16 Sasa jambo lingine tunaloamini, ni kwamba, “Kila mmoja hupewa Roho wa kufaidiana.” Sasa, tunaamini ya kwamba wakati karama hizi, na kadhalika, zinapofanya kazi Kanisani; ambazo tunazitaka sana na tungetaka kwamba watu waliokarimiwa, na Roho, waje wakaabudu pamoja nasi.

17 Sasa, karibu kila mahali, tunaona ya kwamba wakati hizi karama zinapokuwa katika watu, hao watu hawafahamu *vipi* wala ni *wakati gani* watatumia karama hizi, na kwa kufanya hivyo, wao huleta shutuma; ambavyo tunaamini ndivyo tu Shetani angetenda kuwafanya watu walio nje, hao wasioamini, na kadhalika, waogope hii Baraka ya ajabu ambayo Mungu amelipa Kanisa siku hizi.

18 Paulo alisema, “Akija mgeni kati yetu, nasi sote tunanena kwa lugha, je, mtu huyo hataondoka na kusema sisi ni ‘wenda wazimu’? Bali mmoja akitabiri na kufanya wazi siri za moyoni, basi wao wangeanguka chini na kusema, ‘Mungu yu kati yenu bila shaka.”

19 Basi, tunaamini ya kwamba karama za za kiroho, miongoni mwa waamini, ni jambo la kawaida. Hatuwezi kuamini ya kwamba mtu anaweza kuhubiri chini ya Upako na (basi) awe mwalimu aliye na upako, kisha akane karama ya uponyaji, ama karama ya unabii, ama kunena kwa lugha, ama kufasiri lugha, ama moja ya karama hizi zingine.

20 Kwa hivyo, basi, hivi ndivyo ninavyoamini Neno la Mungu, jinsi Maskani ya Branham, kwenye Barabara ya 8 na ya Penn hapa Jeffersonville, yanavyopaswa kuendeshwa. Nafikiri, jambo la kwanza, naamini ya kwamba mambo haya ninayosema ni muhimu na hayana budi kutekelezwa kwa njia hii, katika Maskani ya Branham, ili yapate kufanikiwa katika Bwana. Na endapo wakati wo wote haya, hili, litaulizwa, mtu aliye

na swali hilo juu Yake anaweza kutaka shauri kwangu iwapo hawezi kumpata mchungaji, ama wanaweza kumtaka shauri mchungaji. Endapo niko nyumbani, toka safarini, nitafurahia ku—kumsaidia mmoja wa wa shiriki au mchungaji wakati wo wote. Na mambo haya ni kulingana na Maandiko, nami naamini ni utaratibu wa Kanisa.

21 Nafikiri, kwanza, ya kwamba kila mshiriki, au kila mwabudu, wa Maskani ya Branham, inawapasa kupendana sana kwa upendo wa Kiungu hata (ingekuwa) mioyo yao ingekuwa na shauku sana ya kuonana inapowapasa kuondoka, kupumukana kwenye ibada, usiku. Mimi naamini hasa katika "upendano wa Kiungu." Mtume Paulo alisema ya kwamba hiyo ilikuwa bayana ya Roho Mtakatifu. "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu," kasema Yesu, "mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Nasi tunaamini ya kwamba ni upendo wa Mungu uliomtuma Yesu Kristo duniani, kufa kwa ajili yetu sote. "Mungu aliupenda ulimwengu, akamtoa Mwanaye pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali atakuwa na Uzima wa milele." Na *Uzima* wa milele hapa ni "Uzima wa Mungu Binafsi," kwa sababu tunafanyika wana na binti za Mungu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu; ambaye ni Uzao wa Ibrahimu, na anatupa imani ambayo Ibrahimu alikuwa nayo, alipomwamini Mungu kabla hata hajatahiriwa.

22 Sasa, jambo linalofuata, tunaamini ya kwamba hawa waabudu wanapaswa "kukutanika pamoja, hawa wenye hizo karama," kama vile lugha, na hao watu wanaopata funuo na mafasiri, na kadhalika. Hawa washiriki, ama hawa waamini, hasa, wanapaswa kukutanika yapata dakika arobaini na tano ama saa moja kabla ibada hazijaanza. Kanisa linapaswa kufunguliwa mapema, nao waamini wakutanike pamoja katika siku hizi usiku, yapata dakika arobaini na tano hadi saa moja kabla ibada hazijaanza.

23 Naamini, Maskani ya Branham wakati wote yanapaswa kuwa na mpiga piano aliyejazwa na Roho, ambaye atakuja mapema, amejazwa na Roho Mtakatifu, naye angepiga muziki wa kiroho pole pole sana, kama vile "Msalabani pa Mwokozi, hapo miliomba upozi; akaniokoa kwa Damu, Mwana wa Mungu!" Kitu kama hicho. "Karibu na Wewe, Mungu wangu." "Mwamba Wenye Imara, Kwako Nitajificha." Ama, "Karibu na Msalaba," ama kitu kama hicho; kwa sauti dogo, pole pole, anapotafakari daima katika Roho Mtakatifu, mwanamume ama mwanamke, ye yote yule.

24 Ndipo ninaamini ya kwamba waabudu, wanapoingia, wanapaswa kulakiwa, kisha watundike makoti yao na kofia zao, waonyeshwe viti vyao kwa ukarimu ambao unawezekana tu kwa mabawabu au mashemasi waliojazwa Roho Mtakatifu, na katika upendo, kuona kwamba Kanisa la Mungu aliye hai linaendelea.

25 Hawa waabudu hawapaswi kuzungumziana, na kuzungumza na walio upande wa pili, na kupiga kelele kanisani.

26 Wao wanapaswa kukutanika pamoja. Kwanza, waingie ndani pole pole wakiomba kimoyomoyo, labda kwenye madhabahu, kwa dakika chache. Si kuomba kwa sauti kubwa; utamkatiza mtu mwingine; maombi ya kimoyomoyo, uko katika kuabudu, Hebu lididimie ndani. Unaabudu, rohoni mwako, kisha unarudi kitini mwako.

27 Ama, si lazima uende madhabahuni. Nenda tu uchukue kiti, uketi chini, usikize muziki; ufunge macho yako, uinamishe kichwa chako; na, huku umenyamaza kimya ukimwabudu Mungu, wakati wote.

28 Kisha kama Roho akimfunulia mtu mwingine jambo fulani, ama—ama mtu mmoja ajazwe na Roho kufikia mahali ambapo watanena kwa lugha, basi mtu huyu anapaswa kuinuka na kutoa huo ujumbe. Na kila mtu hana budi kutulia hata fasiri itakapokuja.

29 Fasiri itakapokuja, haipaswi kuwa ni kunukuu Maandiko, ama—ama jambo lisilo na maana. Haina budi kuwa ni ujumbe kwa Kanisa, ama tunafikiri ya kwamba hiyo ingekuwa katika mwili, tunaona mengi sana ya hayo. Na sasa, kama ninavyoamini, Ro—Roho alikuwa tu akinena kwa ajili ya "kulijenga Kansia."

30 Basi sasa huenda ukawa ujumbe wa namna hii, labda. Labda watu wanakusanyika wakati huu, wagojwa wamekuja. Labda kuna mtu aliyelala, amepooza ama cho chote kile. Haujapata kumwona hapo mbeleni. Bali fasiri itakapokuja, ama yule ambaye amenena hivi punde, angesema, "Vema, BWANA ASEMA HIVI, huyu mtu aliye miongoni mwetu ametoka mahali *fulani na fulani,"* na aeleze mahali hapo. Naye angesema, "Yeye amepooza kwa sababu, miaka mitatu ama minne iliyopita," cho chote kile, "yeye alifanya uovu fulani," kitu kama, "alimwacha mke na watoto wake, kisha akawatoroka. Naye akaanguka toka juu ya lori," na kitu kama hicho, "naye akajeruhiwa, akapooza. BWANA ASEMA HIVI. Iwapo atatubia hilo, naye ataahidi kumwendea mkewe na kupatana naye, basi ataponywa sasa hivi na kuirudia jamaa yake."

31 Na kabla mtu ye yote hajasema jambo lo lote, hapana budi pawe na yapata watu wawili, au zaidi, mtu ama watu jengoni, ambao wamekomaa kiroho katika Mafundisho ya Injili, ambao wana utambuzi mzuri wa roho, watainuka na kusema ya kwamba "Ni wa Bwana."

32 Na iwapo jambo hili halitatendeka, basi lugha hazipaswi kutajwa kanisani. Kama mtu huyo akinena kwa lugha, Paulo alisema, "Iwapo hapana mwenye kufasiri," na kadhalika, "basi na wanene nyumbani," ama po pote walipo, "kwa maana wao wanajibariki nafsi zao tu, na si kwa ajili ya kulijenga Kanisa."

33 Na mtu huyu, baada ya kunena, na kufasiriwa, kisha wapambanuzi wawili ama watatu, kulingana na Mafundisho ya Mtakatifu Paulo, ya Biblia, ya kwamba haina budi "kupambanuliwa na wapambanuzi wawili ama watatu."

34 Basi hebu huyo mtu aliyeitwa Naye, aende. Na huenda ikawa Yeye atamchagua mtu fulani, au mchungaji au mtu mwingine, aende akamwekelee mikono mtu huyu, na ya kwamba huyo aliye mgojwa au anayeteseka, wao watapata afya. Basi hebu mchungaji ama huyo mtu mwingine, ye yote yule aliyechaguliwa na Roho Mtakatifu kuenda "kuomba kwa imani," hebu wao waende wakamhudumie mtu huyo kulingana na yale Roho amesema. Ndipo wakati huo, mtu ambaye. . .Na cho chote alichosema Roho Mtakatifu, kitatendeka, mara hiyo basi, jinsi tu Roho Mtakatifu alivyosema.

35 Ndiposa watu wanaweza kufurahi, kutoa shukrani, na kumsifu na kumwabudu Mungu, maana Mungu anataka kuabudiwa.

36 Kisha hawana budi, ndipo hawana budi kuviinamisha vichwa vyao na kuomba tena, kuona kama kuna ujumbe mwingine ambao Roho Mtakatifu angetaka karama hizi zidhihirishe, mbele.

37 Ndiposa iwapo mtu ye yote atanena kwa lugha wakati wo wote, na kufasiriwa, nao—nao wapambanuzi watamtuma mtu huyo kuchukua, kufanya cho chote alichoambiwa afanye, na isipotimia, basi kundi hilo lote litaondoka liende madhabahuni na kumwomba Mungu aondoe huyo roho toka kwao, kwa kuwa hamna mtu ye yote angalitaka roho kama huyo. Tungejua ni wa uongo, na ni wa adui, wala si wa Mungu kwa maana Mungu aweza tu kusema ukweli pekee. Hebu kanisa lielewe hilo dhahiri sana na kanisa, kabla hamjaanza huu, utaratibu huu mpya.

38 Kisha, labda, huenda ikawa kitu kama hiki, ujumbe huo ungemwambia ndugu fulani, labda ambaye, tuseme, "Aliishi karibu na barabara ya reli," ama po pote pale, "ahame huko, kwa sababu kutakuwa na ajali haya humo barabarani," ama cho chote kile, kitu kama hicho.

39 Basi hebuni wapambanuzi, baada ya kuliruhusu kanisa kunena, ama kutekeleza ujumbe huu ambao umetolewa hivi sasa, iwapo uamuzi wao ni, "Ni wa Mungu," basi angalieni muone kama itatimia.

40 Na itakapotimia, basi mshukuruni Mungu, na muwe wema, muwe wema mioyoni mwenu Kwake. Ndipo mumpe sifa na kumwabudu, na muwe wanyenyekevu. Zaidi ya yote, iweni wanyenyekevu.

41 Msije mkajidai hata kufikia mahali ambapo mnajua mengi zaidi juu yake kuliko mchungaji wenu ama kanisa ambalo mnaabudia. Mkifikia mahali hapo, basi ningewaulizeni kila mmoja wenu kutafuta mahali pengine pa kuabudia. Kwa sababu

minamuuliza mchungaji asikubalie kamwe cho chote nje ya utaratibu wa Biblia, jinsi tuonavyo humu kanisani. Halafu tunataka karama hizi ziendelezwe, jinsi ipasavyo, na waabuduo. Kama zikiendelezwa ipasavyo kulingana na Neno, mtaona kanisa la ajabu na lenye nguvu likitenda kazi kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo.

42 Sasa, jambo jingine litakalotendeka, litakuwa ya kwamba iwapo hawa watu ambao wanazo, wanaotoka nje ya utaratibu katika nyakati hizi, ya kwamba shemasi ama bawabu aliyejazwa na Roho Mtakatifu na ana neema nyingi moyoni mwake, atamwendea mtu huyo, kwa uchaji, kama baba, naye atawasahihisha hivi. Ama, mchungaji, ye yote yule, ambalo lingepaswa kufanywa na shemasi; kwa maana mchungaji, wakati huu, wakati ibada hizi za kiroho zinapoendelea, anapaswa kuwa kwenye chumba cha maombi, ama mahali pengine, akiomba.

43 Jumbe hizi, Basi, iwapo hamna jumbe zinazotolewa, hamna funuo, basi watu wangeruhusiwa, kama walitaka, kuinuka na kutoa ushuhuda, ushuhuda tu kwa utukufu wa Mungu. Si lazima wafanye hivyo, bali shuhuda zinapaswa kutolewa kabla ya ujumbe ama ibada yo yote ya nyimbo haijaanza, ama cho chote kile, shuhuda katika ibada hizi za kuabudia.

44 Je, mnafahamu, kanisa, ya kwamba katika kufanya hivi, kanisa lote liko katika roho wa kuabudia, kabla Neno halijatolewa kufundishwa. Kisha Roho Mtakatifu anachukua hilo Neno, na kumdhihirisha Mungu kwa Neno, lipate kuwa dhirisho la ibada yenu.

45 Sasa, baada ya haya, ni wakati wa mchungaji kuja. Iwapo kuna ujumbe unaoendelea, tuseme . . . Mchungaji apaswa kuingia, tuseme, saa moja na nusu kamili, na, ama saa mbili kasorobo. Na iwapo hizi jumbe zingali zinaendelea, kabla mchungaji hajaingia katika . . . hajatoka kwenye chumba chake cha kusomea, ama po pote alipo, kuchukua mahali pake jukwaani; ndugu fulani anapaswa kumshauri, kwa maana watakatifu wanajua ya kwamba mchungaji anapokuja jukwaani, ni wakati wa ibada. Na hiyo inatoa wakati mwingi na wa kutosha kwa ajili ya kudhihirishwa kwa karama, kumleta Roho wa Mungu katika ku—kusanyiko.

46 Na iwapo mtu asiyeamini ye yote atakuwa pale, huku anafanya fujo; mtu mwenye moyo mwema atamwendea, kama bawabu ama shemasi, na awaambie ya kwamba walikuwa—wanaombwa kuwa wenye kicho, ama wawe na kicho ibada inapoendelea kwa maana, Roho yuko katika hilo jengo, na karama za Mungu zinadhihirishwa kwa ajili ya kulijenga Kanisa. Na mtu huyu hana budi kuambiwa katika upendo, na si katika hasira. Isipokuwa ifikie mahali ambapo walikuwa wakinywa pombe, ama wengine kutokutii, ama cho chote

kile ambacho kingekatiza ibada ya—ya Bwana, ambamo hizo karama zinadhihirishwa, basi mtu huyo anapaswa, anahitajika, anapaswa kupelekwa kando, katika moja ya vyumba vya nyuma, ama po pote pale, akazungunziwe, na kushughlikiwa, kwa upendo.

47 Sasa, mchungaji anapokuja jukwani. Wakati mchungaji anapokuja jukwaani, ningeshauri, katika Maskani ya Branham hapa, ya kwamba mchungaji aongoze kusanyiko katika angalau wimbo mmoja ama mbili zilizo nzuri. Kwa maana tumeona ya kwamba, ya kwamba wakati watu wengi sana wanapojaribu kuongoza kanisa, inazusha tu shida. Ningeshauri, kama nilivyofanya nilipokuwa mchungaji humu kanisani, niliongoza nyimbo, mimi binafsi. Nami naona ya kwamba ni jambo nzuri iwapo mchungaji atafanya hivyo, yeye binafsi.

48 Na katika mikutano yote ya maombi, po pote wanapokusanyika, makundi-makundi, mkutano wa maombi, mchungaji hana budi kuwa katika kila mmoja wao. Hiyo isiachiliwe mtu mmoja binafsi kuongoza mikutano kama hiyo. Kwa maana tumeona ndivyo ilivyo, ya kwamba wao huenda kombo, katika mafundisho, nao wanasababisha, na kuyarudisha kanisani, na mara nyingi, wanasababisha uzushi, na kadhalika, ambao si mali ya Kanisa la Mungu aliye hai. Basi mchungaji anapaswa kuhudhuria mikutano yote ya maombi, na kadhalika, walipo kusanyiko au waumini.

49 Naye mchungaji hapaswi kamwe kuchagua upande mmoja katika mkutano, kwa kusema kuna kundi moja hivi na lingine *vile*. Mchungaji anapaswa kuwa kati ya wote wawili, na kuwaendea, na kuwapatanisha, mara moja. Na iwapo hawezi kuwapatamisha, hebu na aondoke aende pamoja na shemasi mmoja. Ndiposa kama hawatamsikia mchungaji wala shemasi, basi hayo yanapaswa kuambiwa kanisa, kisha, kama Yesu alivyosema, "Na awe kwenu kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru." "Na lo lote mtakalofunga duniani," kasema Yesu, "Nitalifunga Mbinguni, na lo lote mtakalofungua duniani, nitalifungua Mbinguni."

50 Sasa, mchungaji anapokuja jukwaani, hebu mchungaji basi aongoze, angalau, wimbo mmoja ama nyimbo mbili, kisha aliendee Neno moja kwa moja.

51 Hamna wakati kwa hii mikutano mirefu ya ushuhuda, huku kila mtu anasimama, na kusema neno. Hilo halifanikishi Maskani ya Branham.

52 Endapo watu wo wote, iwapo mnasikiza ukanda huu, na ninyi, imefanikiwa kanisani mwenu, vema, hiyo ni sawa kabisa. Nasi tunafurahia hayo sana, ya kwamba inafanikisha kanisa lenu.

53 Bali katika letu, haifanikishi, inasababisha tu mchafuko. Nimekuwa mchungaji humu miaka ishirini na kitu, nami

nimeona kwamba inasababisha tu mchafuko. Iwapo una ushuhuda, utoe hapo mbeleni, katika kusanyiko la watu, huku Roho yuabariki, na kadhalika.

54 La, sivyo, njia halisi ya kushuhudia, si kanisani, ni kule nje mahali penye giza. Hebu Nuru yako iangaze palipo na giza. Nenda kwenye vilabu vya pombe, na ambapo dhambi na kadhalika inalundikana, kisha acha Nuru yako ipaangazie. Hapo ndipo mahali pafaapo.

55 Bali, hata hivyo, iwapo Bwana amekubariki na kukupa baraka maalum, ama jambo fulani unalopaswa kuwaambia watu, fanya hivyo wakati wa ibada hiyo nyingine, ibada ya kwanza, ibada ya utangulizi, ama wakati Roho anapowabiriki na kutolewa kwa ushuhuda na funuo, na lugha na fasiri, na kadhalika, katika wakati wa kuabudu, wa watakatifu, kabla Neno la Mungu halijaletwa.

56 Mchuagaji, baada ya kuongoza wimbo huu, ataliongoza kanisa katika maombi mara moja, na maombi ya kusanyiko, yeye binafsi, anaposimama jukwaani, akiwauliza wengine wote kuinamisha vichwa vyao katika maombi.

57 Hii tumeiona kuwa ni baraka kuu sana, na njia bora sana ya kuliendeleza kanisa.

58 Halafu, jambo lingine ambalo mchungaji anapaswa kufanya basi, baadaye. Iwapo walikuwa na mkutano halisi wa kiroho, huku karama zikidhihirisha siri nyingi za mioyo ya watu, na mambo ambayo yanapaswa kufanywa na karama katika mkutano huo; basi Roho wa Mungu yumo katika huo mkutano, na ni rahisi sana basi kwa mchungaji kumpata Roho wa Mungu (ambaye tayari yumo katika huo mkutano) katika Neno la Mungu, anapolisoma na kuanza kuhubiri. Mchungaji basi ahubiri cho chote Roho Mtakatifu angeweka moyoni mwake, cho chote anachotaka kufanya, akisimama pale.

59 Bali kusanyiko. . . Wanaweza kufurahi, anapohubiri, bila shaka, ama kusema "amina" Neno linapokuja. Lakini, kuhusu kuinuka na kutoa u—ujumbe katika lugha na kufasiri, huku Roho Mtakatifu anatenda kazi kupitia kwa mchungaji, Maandiko yanapinga hayo, na yalisema, "Roho wa nabii humtii nabii."

60 Mchungaji basi hana budi kumwita huyu mtu, na kumwomba awe na kicho na kukaa mahali pake. Mchungaji anapaswa kuwa mtu mnyenyekevu sana, bali si mnyenyekevu sana ila apate kuwa kama Bwana Yesu Kristo wakati Yeye alisokota kamba akawafukuza kanisani. Na sasa Kanisa la Mungu ndilo mahakama makuu sana, na mchungaji ndicho cheo kikubwa sana Kanisani. Mzee ndilo jambo kuu sana katika Kanisa la kimitume, nje ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu huleta Ujumbe Wake moja kwa moja kwa mzee, naye mzee analitoa kwa watu.

61 Watakatifu na karama zao watakuwa na mahali pao, kwanza, kuabudu na kukusanyika pamoja, ambalo, ambalo huleta (kama nilivyokwisha kusema hapo awali) Roho wa Bwana katika jengo hilo, kwa ajili ya mchungaji. Na hiyo inaifanya rahisi sana kwa Roho Mtakatifu kutenda kazi kupitia kwake basi, wakati mkutano mkubwa wa kiroho umekwisha kutangulia mafundisho yake; kisha Roho Mtakatifu anaingia kwa Neno na kufundisha Neno; tayari amekwisha kudhihirishwa kwa karama.

62 Ndiposa wito wa madhabahuni unafanywa basi, baadaye, na wengi wakati huo wataona na kujua, kulingana na kutenda kwa Roho Mtakatifu, na Neno la Mungu ambalo mchungaji analiweka Kwake, ya kwamba ninyi ni Kanisa la Mungu aliye hai. Na kama alivyosema Paulo, wa kale, "Ataanguka kifudifudi na kukiri ya kuwa 'Mungu yu kati yenu bila shaka."

Sasa katika mambo haya, hebu na itendwe katika kicho.

63 Na sasa kwa mchungaji, kwa Ndugu yetu Neville, wakati huu. Kumbuka, yeye ndiye kiongozi wa kanisa hili. Ndugu Neville ana haki ya kutumia mamlaka yo yote ambayo Roho Mtakatifu, cho chote ambacho Roho Mtakatifu angemwambia kusema, kwa maneno mengine. Kanisani, yeye ana haki kwa cho chote ambacho Mungu angelimwongoza kufanya. Yeye pia ana haki juu ya halmashauri ya mashemasi, ama wadhamini, ama—ama mpiga piano, ama afisi yo yote ile ya kanisa ambayo anataka kubadilisha, akijisikia anaongozwa na Roho Mtakatifu kufanya hivyo. Na lo lote afanyalo, nitalitambua, kwa kuwa yeye (naamini) ni mcha Bwana. Nitalitambua kwamba linatoka kwa Bwana, nami nitaliidhinisha jambo hilo, kwa hivyo inampa mamlaka kuliendeleza kanisa jinsi anavyojisikia akiongozwa kufanya. Sasa, ama, afisi yo yote kanisani, ambapo yeye anataka ku—ku—kubadilisha kazi za watu, yeye ana mamlaka ya kufanya hivyo. Ambayo, natumaini ya kwamba hili daima litakuwa la kupendeza na hayo hayatatumiwa kamwe.

64 Basi Bwana na awabariki ninyi nyote. Nami natumainia ya kwamba haya yatatekelezwa vizuri mjuavyo. Na Roho Mtakatifu amlinde kila mmoja wenu.

65 Hebu kila afisa wa kanisa atekeleze wajibu wake, akijua hivi, ya kwamba Mungu atakupasisha jinsi ulivyotekeleza afisi yako kanisani. Kila mtu itamlazimu kutoa hesabu.

66 Nao wafuasi, nao hao watakatifu waliokirimiwa walio kanisani mwetu, wale ambao—ambao hutoa unabii, ama hunena kwa lugha, ama kufasiri, ama wana funuo, sisi tuna furaha sana kuwa pamoja nanyi katika ibada. Nasi tutashirikiana nanyi kabisa katika kila jambo ambalo Roho Mtakatifu atathibitisha ya kwamba amewaambieni. Nasi tunawapenda. Nasi tunaamini ya kwamba hizi karama zimo ndani yenu, na, kama mna nafasi nzuri, na kuziendeleza Kimaandiko, ya kwamba nitakuwa

wafanyi kazi wakuu kati yetu. Basi Bwana na awabariki nyote, ndilo ombi langu la moyoni.

67 Wakristo, tangu nilipousikia ukanda huu, naona niliacha jambo moja, na hilo ni hili; ya kwamba, watu wanaponena kwa lugha, haina budi iwe katika zamu ya "wawili ama watatu," kulingana na Maandiko. Hiyo ni kusema, ni jumbe mbili tu ama tatu zinazopaswa kutolewa katika kila ibada. Hilo ni kulingana na Maandiko ya kwamba "Hizi zamu hazina budi kuwa mbili pekee, ama tatu." Basi tekelezeni mambo haya, ipasavyo, jinsi Roho Mtakatifu ameagiza katika Biblia Yake. Na hivi ndivyo, nijuavyo mimi, inavyopaswa kufanywa. Paulo alisema, "Na iwe zamu kwa zamu, wawili ama watatu, wanaponena." Bwana awabariki.

*Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa*, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org